# ILEMELA YETU

Jarida la Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela

**TOLEO MAALUM**
**MIRADI YA BOOST**

**HALIUZWI**

# MRADI WA BOOST WAIBUSTI ILEMELA

- »» **Shilingi bilioni 1.57 Zilipokelewa kwa ajili ya ujenzi**
- »» **Vyumba 54 vya madarasa, Majengo Mawili ya Utawala, Ofisi Moja ya Walimu, Vyoo Matundu 70 vimejengwa.**
- »» **Madawati 1075 kwa wanafunzi wa Elimu Msingi, Meza na Viti 90 kwa ajili ya Wanafunzi wa Elimu Awali, Viti na Meza 74 kwa ajili ya Walimu, Miundombinu ya Viwanja vya Michezo**




**Mhe. CPA Amos Makalla akizindua shule mpya ya Msingi ya Buteja iliyojengwa kwa fedha za Mradi wa BOOST katika kata ya Kahama**

*ILEMELA NI YETU, TUSHIRIKIANE KUIJENGA*

# TAHARIRI

Msingi wa elimu bora kwa jamii huanzia elimu ya awali na kisha elimu ya msingi. Na elimu iliyo bora itapatikana iwapo tu kuna mazingira bora ya kujifunzia na kufundishia na kama mazingira bora yatakosekana inaweza kupelekea utoro kwa wanafunzi shuleni, ufaulu mdogo , na walimu kukosa umakini wa kufundisha hivyo kupelekea kuwa na jamii ambayo haijaelemika.

Changamoto mbalimbali zimekuwa zikiikabili sekta ya elimu nchini Tanzani hususan sekta ya elimu msingi zikiwemo upungufu wa vyumba vya madarasa hivyo kupelekea msongamano wa wanafunzi madarasani, wanafunzi kutembea umbali kufuata elimu kutokana na kukosekana kwa shule karibu na maeneo wanayoishi, na walimu kutokufundisha kwa ubora unaotakiwa kufuatia mazingira duni ya kufundishia.

Kwa kuliona hilo Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan, iliamua kuja na mradi wa BOOST uliolenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia na kufanikisha upatikanaji wa Elimu Bora ya Awali na Msingi nchini.

Sambamba na hilo kupitia mradi huu wa BOOST Serikali imelenga kupunguza msongamano wa wanafunzi katika shule na kuwezesha wanafunzi kukaa kwa uwiano sahihi wa idadi ya wanafunzi katika vyumba vya madarasa. Aidha mradi huu umeongeza idadi ya samani za wanafunzi na walimu ikiwemo madawati, viti, meza na kabati. Pia kuweka mazingira rafiki kwa wanafunzi kama vile maeneo ya kuchezea (viwanja) na bembea kwa wanafunzi wa Elimu ya Awali.

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ni Miongoni mwa Halmashauri zilizoidhinishiwa Fedha za utekelezaji wa Mradi wa BOOST katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023, ambapo ilipokea kiasi cha Tshs 1,574,000,000.00.(Shilingi bilioni 1.57)

Kupitia fedha hizo Shilingi bilioni 1.08 zimejenga shule mbili mpya za msingi na awali, shilingi milioni 400 zimejenga vyumba 16 vya madarasa katika shule nne za msingi, shilingi Milioni 69.1 zimetumika kujenga vyumba viwili vya madarasa ya mfano elimu ya awali na shilingi milioni 25. 2 zimejenga matundu 12 ya vyoo katika shule 4 za msingi. Pamoja na ujenzi huo yamepatikana madawati 1075, viti na meza 90 vya Elimu ya Awali, viti na meza 74 za walimu.

Hakika mradi wa BOOST umeibusti Ilemela kwani sasa wanafunzi waliokuwa wakitembea umbali mrefu kwenda kutafuta elimu katika kata za Kahama na Buswelu sasa wanafika mapema na kufurahia masomo yao, sio hilo tu bali BOOST imeibusti Ilemela kwa kupunguza msongamano madarasani hivyo imeboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, pamoja na hayo yote jamii ambapo mradi ulikuwa ukitekelezwa waliufurahia kwani walipata ajira hivyo kuongeza kipato chao na kujifunza namna ya kusimamia miradi ya maendeleo na kuweza kuimiliki.

Sisi wana Ilemela sote kwa pamoja tunatoa heko na kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyotoa kipaumbele katika sekta ya elimu nasi wana Ilemela tunamuahidi kuwa tutaitunza miundombinu ya elimu,pamoja na kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kuanza shule wanaripoti shulen pamoja na kuhakikisha walimu wanafundisha kwa bidii na kutoa elimu iliyo bora.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KAZI IENDELEE**



# YALIYOMO


01 Rc Makalla Aipongeza Ilemela Ukamilishaji Wa Mradi Wa Boost

03 Wasemavyo Ilemela Kukamilika Kwa Ujenzi Wa Miundombinu Elimu Msingi Kupitia Mradi Wa BOOST

05 Shule Mpya Ya Awali Na Msingi Buteja Kata Ya Kahama

07 Shule Mpya Ya Awali Na Msingi Busenga Kata Ya Buswelu

09 Shule ya Msingi Chasubi-Madarasa Mawili ya awali

10 Shule ya Msingi Igombe-Madarasa Manne

11 Shule ya Msingi Nyamwilolelwa-Madarasa Manne

12 Shule ya Msingi Nyamadoke-Madarasa Manne

13 Shule ya Msingi Nyamhongolo-Madarasa Manne

14 Picha Mbalimbali Mradi wa BOOST



# RC MAKALLA AIPONGEZA ILEMELA UKAMILISHAJI WA MRADI WA BOOST

*Picha na Habari Na*
*Kitengo cha Mawasiliano*

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe CPA Amos Makalla ameipongeza Manispaa ya Ilemela kwa kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya elimu msingi kupitia mradi wa BOOST na kusema kuwa ameridhishwa na utekelezaji wa mradi huo.

Mhe.CPA Amos Makala ametoa pongezi hizo wakati wa hafla ya makabidhiano ya ukamilishaji wa miradi wa BOOST iliyofanyika tarehe 13 Septemba 2023, ambayo ilienda sambamba na .uzinduzi wa Shule mpya ya Msingi ya Buteja ambayo nayo imejengwa kwa fedha za BOOST

Akiongea na wananchi waliofika kushuhudia makabidhiano hayo, amesema kuwa katika Mkoa wa Mwanza Ilemela imekuwa ya kwanza kukabidhi mradi huu wa BOOST na kusema ina maanisha Ilemela inazungumza lugha moja, ameongeza kusema kuwa amekagua madarasa na ameridhishwa nayo.
"Ilemela mmekuwa wa kwanza kukamilisha na kukabidhi mradi huu wa BOOST kwa Mkoa wa Mwanza,maana yake hapa chama na serikali lugha yenu ni moja.Niwashukuru kwa kazi nzuri mliyofanya, nimeenda kwenye madarasa nimeona madawati mazuri nimeona hadi meza na kiti ch mwalimu nimepita sehemu nyingi sijawahi kuona na nimeliona Ilemela kwa mara ya kwanza", alisema Mhe Makalla

Sambamaba na hilo CPA Makalla amesema kuwa Serikali imetoa fedha nyingi ya ujenzi wa miundombinu ya elimu mkoani Mwanza, hivyo amewataka wazazi, walezi, walimu na wanafunzi kuhakikisha kuwa utoro haukubaliki Mwanza na kuwa watoto wote wanapaswa kwenda shule.

"Madarasa haya hayatakuwa na maana kama mtoto haendi shule hivyo tuudhibiti utoro sisi wote wanafunzi, wazazi, walimu na walezi wote ni wadau wa kushughulika na suala la utoro", Alisema CPA Makalla.



Akimkaribisha Mkuu wa Mkoa, Mhe Hassan Masala Mkuu wa Wilaya ya Ilemela pamoja na kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa fedha alizotoa kutekeleza mradi huu amesema kuwa Wilaya ya Ilemela itaanza kuyatumia madarasa hayo mara tu shule zitakapofunguliwa mwezi huu wa tisa 2023.

"Tumekubaliana sisi kama wilaya madarasa haya 54 yaanze kutumika wiki ijayo punde shule zitakapofunguliwa." Alisema Mhe. Masala

Nae diwani wa kata ya Kahama Mhe.Samwel Buchenja amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kusema kuwa ujio wa shule hii utawezesha mitaa kama mitatu Lukobe,Buteja na Kadinda na kata ya jirani ya Buswelu kunufaika na ukaribu wa shule hiyo kwa kuondoa adha ya watoto kutembea umbali mrefua kufuata shule.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa mradi wa BOOST, Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela Adv. Kibamba Kiomoni amesema kuwa lengo kuu la mradi huu wa BOOST ni kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia na kufanikisha upatikanaji wa elimu bora ya awali na msingi sambamba na kupunguza msongamano wa wanafunzi na kuwezesha wanafunzi kukaa kwa uwiano sahihi wa idadi ya wanafunzi katika vyumba vya madarasa.

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ilipokea kiasi cha shilingi 1.57 fedha kutoka Serikali Kuu kupitia mradi wa BOOST ambazo zimetumika kujenga vyumba 54 vya madarasa, vyoo matundu 70, majengo 2 ya utawala, ofisi moja ya mwalimu, madawati 1075, viti na meza 90 vya Elimu ya Awali, viti 74 na meza 74 za walimu, na miundombinu ya viwanja vya michezo.









# WASEMAVYO ILEMELA KUKAMILIKA KWA UJENZI WA MIUNDOMBINU ELIMU MSINGI KUPITIA MRADI WA BOOST

Kufuatia kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya elimu msingi iliyojengwa kwa fedha za mradi wa BOOST, wananchi wa Ilemela wamemshukuru Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuboresha sekta ya elimu hususan Elimu Msingi.

## MHE.CPA AMOS MAKALLA RC MWANZA

"Nimekagua madarasa yana ubora wa hali ya juu kwani mazingira ya kujifunzia na kufundishia yameboreshwa kwa kiwango cha juu nimeona madawati mazuri , meza na kiti cha mwalimu, kitakachomwezesha kukaa wakati akiwasimamia wananfunzi, ninadiriki kusema watoto hawa washindwe wenyewe kusoma vizuri na ili kuunga juhudi za Serikali yetu ni wajibu wetu wote; wazazi walezi, walimu ,wanafunzi kuhakikisha kuwa tunadhibiti suala la utoro kwani madarasa haya hayatakuwa na maana ikiwa hakutakuwa na wanafunzi"

## MHE.HASSAN MASALA- DC ILEMELA

"Tulikuwa na uhaba wa madawati zaidi ya 5000 tumeendelea kutatua changamoto hii kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali na kupitia mradi huu tumeongeza madawati zaidi ya 1000 hivyo imesaidia kupunguza changamoto ya upungufu wa madawati nah ii tasiri yake ni kuwa watoto wetu zaidi ya 1000 waliokuwa wanakaa chini ndani ya Manispaa wataenda kukaa kwenye madawati na hivyo kubakiwa na upungufu wa madawati 2000 kwa mujibu wa takwimu zilizopo"

## NDUGU. YUSUPH BUJIKU MWENYEKITI WA CCM WILAYA YA ILEMELA

"Kazi hii iliyofanywa ni kubwa , watoto wetu wanaendelea kutengenezewa mazingira mazuri ya kupata elimu tunaendelea kumshukuru Mhe. Rais kwa jambo hili kubwa na sisi CCM tutaendelea kuunga mkono juhudi zake."

## MHE. RENATUS MULUNGA- MSTAHIKI MEYA WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

"Ukiulizwa Maendeleo ni nini duniani sema ELIMU, Hivyo ninamshukuru sana Mhe DKT SAMIA SULUHU HASSAN, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutuboreshea miundombinu ya Elimu katika Halmashauri yetu, nasi tunaahidi kuendelea kuunga mkono juhudi zake"

## WAKILI KIBAMBA KIOMONI-MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

"Uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela unatoa Shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania MHE. DKT SAMIA SULUHU HASSAN kwa kutoa fedha kiasi cha Shilingi Bilioni 1.57 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule ya Msingi kupitia mradi wa BOOST kwani kupitia ujenzi wa miundombinu hii, utapunguza umbali toka makazi ya wanafunzi na shule ilipo na kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani ahadi yetu ni kuendelea kutekeleza miradi mingine kwa umakini kwa kuzingatia thamani ya fedha na ubora ili jamii iweze kufaidika"

## MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA HUDUMA ZA JAMII ILEMELA

***Mhe Hussein Magera*** ambae ni Diwani wa Kata ya Ibungilo, amemshukuru Mhe Rais na kusema haya, "tutahakikisha fedha zinazokuja zinasimamiwa vizuri na kutumiwa vizuri ili mwisho wa siku tuweze kutatua kero katika jamii na kuleta tija kwa wananchi"

## DIWANI WA KATA YA KAHAMA MHE SAMWEL BUCHENJA

"Nashukuru sana kwa ujio wa shule hii ya Buteja kwani itawezesha mitaa kama mitatu ya kadinda,



buteja lukobe na kata ya jirani ya Buswelu mtaa wa Kigalla, zamani hakukuwa na shule na usumbufu ulikuwa mkubwa hususan mtaa wa Buteja ndio wanufaika wa kwanza, nina imani kabisa kukamilika kwa shule hii kunaenda kuondoa adha ya watoto kutembea umbali mrefu"

Ameendelea kusema kuwa, Shule hii ni ya mfano, Mhe Rais ametutendea haki tunamshukuru kwa hili kwani mara nyingi tunapoelekea mwisho wa mwaka ilikuwa tunaanza kuchangisha wananchi ili kupata fedha kwa ajili ya kuongeza madarasa kwa sasa hakuna sababu ya kuchangisha kwani tuna shule mpya yenye madarasa ya kutosha.

## DIWANI KATA YA BUSWELU, MHE SARAH NGH'WANI

Ameshukuru kwa fedha hizi za mradi wa BOOST kwani ni kwa muda mrefu mtaa wa Busenga ulikuwa na uhitaji wa shule ya msingi na kwa sasa hakuna mtoto wa Busenga na mitaa ya jirani atashindwa kusoma , pamoja na shukrani hizo ameomba kufikiriwa kwa ujenzi wa shule ya sekondari ili kuwasaidia watoto wa Busenga kupata elimu kwa urahisi.

## WALIMU

***Mwalimu Felician Makenzie*** ambae ni Mwalimu Mkuu katika shule ya Msingi Igombe, shule ilikuwa na changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa kwa hatua hii ambayo tumejenga vyumba vya madarasa vinne itatusaidia kupunguza msongamano madarasani na kwa vyoo vilivyojengwa itapunguza foleni na changamoto ziliziokuwepo awali pamoja na hilo tunamuomba Mhe Rais aendelee kutoa fedha ili miundombinu ya Shule za Msingi iendelee kuboreshwa.

***Mwalimu Mectilda Mashimba*** ni Mwalimu mkuu msaidizi katika shule ya msingi nyamadoke, kukamilika kwa madarasa haya yanaenda kuturahisishia hali ya ufundishaji kwa ujumla tulikuwa na msongamano wa watoto ambao walikuwa wanashindwa wajifunzeje kwa sasa watoto watakaa kwenye madawati na kupunguza msongamno madarasani tunamuomba pia alete kwa awamu nyingine ili watoto wapate kusoma vizuri.

## WANAFUNZI

***Goodygladness Gelgodaniel, Joyce James, Fransischo Clavery Magesa, Bryton Emmanuel na Elizabeth Milton,*** ni wanafunzi katika shule za Msingi Igombe, na Nyamadoke katika nyakati tofauti wamemshukuru Mhe Rais kwa kuleta fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya madarasa na matundu ya vyoo katika shule zao kwani ujenzi huo unaenda kupunguza msongamano madarasani hivyo kuwawezesha kusoma vizuri pamoja na kuondoa foleni vyooni na vyoo vilikuwa vinajaa hali iliyokuwa ikiwasumbua, si hivyo tu madawati mapya yatawasidia wanafunzi kusoma katika mazingira bora ,hivyo wamemuahidi Mhe. Rais kuwa watasoma kwa bidi ili waweze kufikia malengo yao kwani wapo wanaotaka kuwa rubani, Rais, Daktari n.k lakini pamoja na hayo wamemuomba aendelee kutoa fedha kuboresha miundombinu ya shule zao

## MWENYEKITI WA MTAA WA BUTEJA

***Mabele Elias*** ni Mwenyekiti wa Mtaa wa Buteja, kata ya Kahama ameshukuru kwa mradi wa BOOST ikiwa ni pamoja na wananchi wa Kahama tuliposikia Mtaa huu unapata shule tulifurahi na tulikuwa tayari kutoa eneo ili shule iweze kujengwa kwani ilikuwa hitaji kubwa la mtaa wetu sasa watoto wataacha kutembea umbali mrefu hivyo kuepusha ajali.

## MWANANCHI WA MTAA WA BUTEJA-KATA YA KAHAMA

***Stella Mazigiruka maarufu kama Mama Nyanjige*** ni Mwananchi wa Mtaa wa Buteja, alikuwa na haya ya kusema;

"Mimi nipo jirani sana na shule hii ilipojengwa tunafurahi sana kwa ujio wa hii shule kwa sababu watoto, wajukuu wetu watasoma Mwenyezi Mungu amtunze Rais wetu shule yetu ni nzuri sana kiasi kwamba watu wakifika wanadhani ni shule ya binafsi hivyo namshukuru Sana Mhe Rais wetu Mama Samia na Mungu amlinde".




***SHULE MPYA YA AWALI NA MSINGI BUTEJA KATA YA KAHAMA GHARAMA: SHILINGI MILIONI 540.30***



***SHULE MPYA YA AWALI BUTEJA KATA YA KAHAMA***






















**SHULE MPYA YA AWALI NA MSINGI BUSENGA KATA YA BUSWELU GHARAMA: SHILINGI MILIONI 540.30**














**SHULE MPYA YA AWALI BUSENGA KATA YA BUSWELU**











# SHULE YA MSINGI CHASUBI








**UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA MAWILI YA MFANO ELIMU YA AWALI**

**UJENZI WA MATUNDU SITA YA VYOO**

**UWEPO WA ENEO LA MICHEZO (BEMBEA)**

**GHARAMA ZA MRADI SHILINGI MILIONI 69.1**





# SHULE YA MSINGI IGOMBE







**UJENZI WA VYUMBA VINNE (4) VYA MADARASA**

**UJENZI WA MATUNDU MATATU YA VYOO**

**MADAWATI 25 KWA KILA DARASA**

**GHARAMA YA MRADI SHILINGI MILIONI 106.30**



# SHULE YA MSINGI NYAMWILOLELWA







**UJENZI WA VYUMBA VINNE (4) VYA MADARASA**

**UJENZI WA MATUNDU MATATU YA VYOO**

**MADAWATI 25 KWA KILA DARASA**

**GHARAMA YA MRADI SHILINGI MILIONI 106.30**





# SHULE YA MSINGI NYAMADOKE







**UJENZI WA VYUMBA VINNE (4) VYA MADARASA**

**UJENZI WA MATUNDU MATATU YA VYOO**

**MADAWATI 25 KWA KILA DARASA**

**GHARAMA YA MRADI SHILINGI MILIONI 106.30**



# SHULE YA MSINGI NYAMHONGOLO







**UJENZI WA VYUMBA VINNE (4) VYA MADARASA**

**UJENZI WA MATUNDU MATATU YA VYOO**

**MADAWATI 25 KWA KILA DARASA**

**GHARAMA YA MRADI SHILINGI MILIONI 106.30**



# PICHA MBALIMBALI MRADI WA BOOST














**HALIUZWI**

**Jarida limeandaliwa na kusanifiwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela**

**SCAN HAPA KUPERUZI TOVUTI YA ILEMELA**


OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA
200BR.YA BUSWELU
33282 BUSWELU
ILEMELA,MWANZA



**Tufuatilie >>>** ilemelamamc | www.ilemelamc.go.tz
Barua Pepe: md@ilemelamc.go.tz